

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO CHA UALIMU BUTIMBA



UJENZI WA LECTURE THEATRE

MKATABA WA UJENZI

A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA

1	MWAJIRI	MKUU WA CHUO CHUO CHA UALIMU BUTIMBA TC S. L. P. 1411 MWANZA KNY: KATIBU MKUU WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA
2	JINA NA ANWANI YA FUNDI (Mwajiriwa)	Jina:..... <u>MATHIAS CHRISTOPHER</u> Anwani:..... <u>MWANZA</u> Simu:..... <u>0762 3949 89</u>
3	ENEO LA UJENZI	CHUO CHA UALIMU BUTIMBA
4	MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI	KUCHOMELEA NA KUFITISHA NGAZI KATIKA JENGO LA UKUMBI WA MIHADHARA
5	GHARAMA YA UFUNDI (+ Skills Development Levy 5% of work service):	TSHS 315,000/= SHILINGI LAKI TATU NA ELFU KUMI NA TANO TUU.
6	MUDA WA MKATABA	Tarehe ya Kusaini. <u>16/05/2022</u>

	(Tangu Kusainiwa kwa Mkataba):	Muda: 30 - SIKU Tarehe ya Kuanza Kazi. 17/05/2022 Tarehe ya Kumaliza Kazi. 16/06/2022
7	MASHARTI YA MALIPO:	<ul style="list-style-type: none"> • Hakuna Malipo ya Awali • Fundi atalipwa kila baada ya sehemu ya kazi husika kukamilika, kukaguliwa na kuthibitishwa.

B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kulingana na maadhibu ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.
3. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
4. Fundi atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na mafundi wote aliowaajiri na kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.
5. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.
6. Fundi atahusika na vitendo (*kama wizi, uharibifu wa mali za chuo*) vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.
7. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.
8. Mwaajiri hatahusika na malipo yoyote kwa mafundi wasaidizi na vibarua.
9. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Mitatu baada ya kazi kukamilika (*Retention Money*) na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.
10. Kiasi cha asilimia 5% kitakatwa na kuwasilishwa mamlaka ya mapato Tanzania (T.R.A) ikiwa ni kwa ajili ya SDL. (*Skills Development Levy 5% of work service*)
11. Ucheleweshaji wa Kazi:
 - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.
12. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

- Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri (kutokana na fedha au vifaa), Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kazi.

13. **Uvunjwaji wa Mkataba:**

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi kupigana au kuonesha viashiria vya aina yoyote ya kuhatarisha kuvunja amani katika eneo la kazi.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanachuo na hatua kali zitachukuliwa.

MWAJIRI:

Saini: [Signature]
 Jina: Mr A MAGIGE
 SIMU: 0768266944
 Cheo: MKUU WA CHUO
 Tarehe: 16/05/2022

CHUO CHA UALIMU BUTIMBA
S. L. P. 1411 MWANZA

FUNDI:

Saini: [Signature]
 Jina: MATIAS CHRISTOPHER
 SIMU: 0762394989
 Cheo: FUNDI
 Tarehe: 16/05/2022

SHAHIDI WA MWAJIRI

Saini: [Signature]
 Jina: Richard A. M. M. M.
 SIMU: 0767928103
 Cheo: MJUMBAHU
 Tarehe: 16/05/2022

SHAHIDI WA FUNDI

Saini: R. Jeeob
 Jina: RICHARD JEEOB
 SIMU: 0767928103
 Cheo: USADIRI
 Tarehe: 16/05/2022